alipomtembelea ofisini kwake Jijini Dodoma, jana.

UHURU UK 16.

# Wafugaji wampongeza Rais Samia kwa kutatua migogoro

Kilosa

**NA WARIOBA IGOMBE**

WAFUGAJI wa jamii ya Kimasai ikiwa ni pamoja na Wakulima wilayani Kilosa mkoani Morogoro wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kitendo chake cha kumaliza changamoto katika wilaya hiyo.

Akizungumza jana wilayani hapa,Daniel Ole Tomas ambaye ni mfugaji alisema wafugaji wa wilaya hiyo wana kila sababu ya kumpongeza Rais Samia kwani mbali na migogoro ya wakulima na wafugaji kuisha lakini pia changamoto nyingi zilizikuwepo zimetatuliwa zote.

"Mimi natoka Kijiji cha Twatwatwa zilichokuwa kikikabiliwa na changamoto lukuki lakini kwa sasa kuna barabara ya kijiji inayopitika kwa urahisi muda wote na pia kijiji chetu kina mawasiliano mazuri kabisa ya simu," alisema Tomas.

Aidha, Tomas aliushukuru uongozi wa shirika la PAICODEO kwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanashirikiana na serikali ya rais Samia Suluhu Hassan kutatua changamoto katika jamii za watu wa Kilosa hususani kakika Kijiji cha Twatwatwa.

Naye, Mkazi wa kijiji hicho, Pili John, alisema anaishukuru serikali pamoja na shirika la PAICODEO kwa misaada mbalimbali ambayo wamekuwa wakiifaya kijijini kwako kwani kumesaidia kuwanyanyua watoto wa kike kielimu.

Pili alisema awali mtoto wa kike aliyekuwa apelekwi shule na badala yake alikuwa anaozeshwa kwa ngo'ombe nyingi lakini kwa sasa suala hilo halipo tena na badala yake watoto wao wakike wanasoma na wengine wanafika elimu ya juu.

"Tunamshukuru sana rais wetu mpendwa ikiwa ni pamoja na PAICODEO kwa ujumla wake kwani sasa tunaona umuhimu wa watoto wetu wa kike kwenda shule tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma kwa kuwaozesha kila mwaka,"alisema Pili.

Aidha, alishukuru kitendo cha kijiji chake kupata huduma ya matibabu kufuatia ujenzi wa Zahanati lakini pia wanawawe wengi kuanza kunufaika na mikipo ya Halmashauri hali ambayo itawafanya wanawake wengi wajiimalishe kiuchumi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa la PAICODEO, Adam Ole Mwarabu, alisema wataendelea kushirikiana na serikali ili kuhakikisha changamoto zilizipo kwenye jamii zinatatuliwa ili wananchi waweze kuendelea na uzalishaji wao wa mali.

Ole Mwarabu alisema kuwa lengo ni kuona wafugaji na wakulima nchini wanaishi vizuri na kwa kueshimiana hivyo shirika lake litaendelea kushirikiana na serikali ili kuhakikisha uzalishaji wa mifugo na mazao unakuwa na tija kwa manufaa ya taifa.

Scanned with CamScanner

MWANANCHI IJUMAA FEBRUARI 11, 2022 MWANANCHI.CO.TZ

Urithi Wetu

**ASILI:** Mkia wa simba ulikuwa bidhaa ya thamani zaidi katika mazoezi ya kuwinda simba



Katika miongo iliyopita, uwindaji simba ilikuwa tambiko, ambalo wanaume walipaswa kupitia

William Shao, Mwananchi

MWANANCHI UK 8.



# Wamasai huua simba kulinda mifugo

Katika toleo lililopita tuliona utamaduni wa Wamasai kuwinda simba na sababu zao za kufanya hivyo.

Hata hivyo, kuna sababu nyingi zaidi ya zile zinazodaiwa kuwa wanawawinda na kuwaua simba ili tu waonekane kuwa ni mashujaa.

Vijana wengi ambao walikuwa wanajiandaa kuingia jandoni walihimizwa katika kutenda jambo hilo. Pamoja na kwamba simba walikuwa wanawindwa zamani, na uwindaji huu umepigwa marufuku katika Afrika Mashariki, bado simba huwindwa wanapoua mifugo, na vijana mashujaa wanaohusika katika mauaji hayo hupewa heshima kuu.

Kutokana na ile hofu ya kwamba idadi ya simba inazidi kupungua, mamlaka za kiserikali zilianza kuingilia suala hilo la uwindaji wa simba.

Simba walikuwa wengi katika maeneo yote ambayo Wamasai waliishi. Maficho yao ya kawaida yalikuwa nyanda zenye nyasi na ndani kabisa ya misitu. Utafutaji wa simba ni kati ya dakika 20 hadi saa 10.

Mashujaa wa Kimasai lazima wamfukuze simba kwa kengele na kumkasirisha. Mchezo huu wa kuwinda uliwakasirisha na kumlazimisha simba kuwakabili wawindaji.

Mbinu nyingine iliyofanikiwa ya kuwinda simba ilikuwa ni kumlazimisha simba aache mnyama aliyemuua kwa ajili ya chakula chake. Njia yoyote kati ya hizi ingeweza kusababisha mapambano na simba.

Kupigana na simba ndani ya msitu ilikuwa changamoto na hatari sana. Simba ni mwerevu sana na anaweza kuruka vichakani haraka kuliko binadamu. Kwa sababu hiyo, wapiganaji wa Kimasai walipendelea kupigana na simba katika uwanda wazi.

Kwa kufanya hivyo, shujaa huyo kulanganya.

Wamasai hawali nyama pori. Wanategemea sana nyama ya ng'ombe, kondoo na mbuzi. Bidhaa tatu hutumiwa kutoka kwa simba aliyekufa: manyoya ya shingoni, mkia na makucha.

Manyoya ya shingoni mwa simba yalikuwa ni mapambo mazuri kwa wanawake wa kijiji na mara nyingi yalitumiwa na mashujaa, hususan maeneo ya mbali kumtambua shujaa hodari.

Baada ya sherehe ya mkutano, shujaa alipokuwa mzee, alilazimika kutupa manyoya ya simba. Kwa kufanya hivyo shujaa alitakiwa kutoa dhabihu ya mwanakondoo wakati wa kuyatupa nyikani manyoya hayo. Tukio hili la dhabihu lilifanywa ili kuepuka roho mbaya. Manyoya hayo yana uhusiano maalumu wa kiroho kwa shujaa. Ilikuwa ni lazima kwa shujaa kuheshimu.

Mkia wa simba ulinyooshwa na kulainishwa na wapiganaji, kisha hukabidhiwa kwa wanawake wa kijiji kwa ushanga. Mkia wa simba ulikuwa bidhaa ya thamani zaidi katika mazoezi ya kuwinda simba. Baada ya kuhitimu, kikundi cha wapiganaji kilikuja pamoja na kutoa heshima yao ya mwisho kwa mikia yote ya simba iliyokusanywa. Mikia ya simba ilitupwa baada ya sherehe ya 'eunoto', yaani sherehe ya "ujio wa umri" mkubwa.

> Takwimu fulani zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 2001 na 2011, morani wa Kimasai waliua zaidi ya simba 200 kusini mwa Kenya.



## Kufuata mkia wa simba

Njia ya kufuata mkia wa simba ilitofautiana kutoka sehemu moja na sehemu nyingine. Kwa mfano, katika sehemu ya Ilkaputiei nchini Kenya, simba alipowindwa, wapiganaji walilazimika kupigana mieleka ili kupata mkia. Aliyeshinda katika mieleka hiyo na kuwa shujaa hodari ndiye hunyakua mkia huo kwa sababu ya ushindi wake. Katika sehemu ya Ilkisonko, ambako ni nchini Kenya pia, mkia ulikwenda kwa shujaa ambaye alikuwa wa kwanza kumrushia simba mkuki.

Mchezo wa kuwinda simba ulihusu kujitolea kwa kundi na mtu binafsi, nguvu, lengo na kujituma. Mchezo ulitegemea historia ya mtu binafsi, mazingira na utamaduni wake.

Wapiganaji hawakuhitaji kuhudhuria mazoezi, wala bunduki kwa ajili ya kuwinda simba. Alichohitaji ni mkuki mmoja na ngao moja tu. Katika historia wako wapiganaji wa Kimasai ambao waliliwa na simba wakati wa uwindaji wao, na wakati huo huo simba wengi waliuawa na wapiganaji hao.

Katika miongo iliyopita, uwindaji simba ilikuwa tambiko ambalo wanaume walipaswa kupitia peke yao au katika kikundi ili wajidhihirishe kwa wapiganaji.

Jamii nyingine hapa nchini zilikuwa zikishughulika na ufugaji tu. Maisha na utajiri wa jamii hizi ulitegemea wanyama. Tangu utoto wao, mafunzo makuu yalihusu ufugaji. Mtoto wa Kimasai alijifunza kuchunga na kulinda wanyama wake tangu utotoni.

Ilimbidi awe askari hodari, aweze kupambana na maadui waliotaka kuteka wanyama wao. Alitakiwa aweze kupigana na wanyama wakali porini wenye kushambulia mifugo. Kumuua simba ilikuwa ni ishara kubwa ya uhodari wa kijana wa kimasai. Mafunzo ya kumwandaa kijana huyo, tangu utoto wake kwa kazi zitakazomkabili katika maisha, yalichukua sehemu kubwa ya malezi.

Kwa maana hii, uwindaji wa simba ulikuwa utamaduni wa kale miongoni mwa Wamasai.

Katika historia yote ya kabila hilo ya miaka 2,000, wapiganaji wake waliwawinda simba ili kulinda mifugo yao na kama sehemu ya desturi yao.

Uwindaji wa simba uliongezeka kadiri idadi ya watu wa eneo hilo inavyoongezeka, huku vijiji na malisho yakisogea zaidi katika makazi ya wanyamapori, na kufanya mifugo ya Wamasai kuwa karibu

...a simba nafasi ya kupambana. ...daji wa simba ulikuwa ni kumpa ...amoto kiumbe mwingine bila

waliomuua simba. Manyoya hayo yalivaliwa na shujaa kichwani wakati tu wa sherehe maalumu na yalisaidia mashujaa wengine kutoka